Sheikh Mash-hur Hasan Āl Salmân

(hafidhahullâh)

NI NANI ALIYEMTANGULIA IMÂM AL-ALBÂNI KUHUSU MAKATAZO YA KUFUNGA SIKU YA JUMAMOSI HATA KAMA LAU ITAANGUKIA KATIKA SIKU YA ĀSHÛRA AU SIKU YA 'ARAFAH?[1]

"KUSWIHI KWA HADÎTH HAKUTEGEMEZWI JUU YA WENYE KUITENDEA KAZI [HADÎTH HIYO], KWAHIYO IWAPO WATU WATAITENDEA KAZI HADÎTH HIYO, BASI HILO NI JAMBO LINALOFAA NA IWAPO WATU HAWATOITENDEA KAZI BASI ITAKUWA NI JAMBO LISILOFAA. VILEVILE, HAPANA HADÎTH YOYOTE ISIPOKUWA PALIWAHI KUWA NA BAADHI YA MA'ULAMĀ NA WATU WEMA WALIOWAHI KUITENDEA KAZI. LAKINI, JUU YA YOTE HAYO, UKOSEFU WA KUIJUA [HADÎTH HIYO] HAKUWAJIBISHI UKOSEFU WA UTEKELEZAJI [KULINGANA NA HADÎTH YENYEWE]. IKIWA SISI HATUIJUI HADÎTH YENYEWE, HILI HALIWAJIBISHI YAKWAMBA HAKUNA ALIYEWAHI KUTEKELEZA KULINGANA NA HADÎTH YENYEWE".

Jawabu kutoka kwa Sheikh Mash-hur (hafidhahullâh):

"... lakini hatahivyo, makusudio ni kwamba, Bârakallâhu fiykum, Sheikh wetu (Imâm al-Albâni, *rahimahullâh*) alikuwa akikataza kufunga siku za Jumamosi, na pindi sisi tulipokuwa tukiulizwa: **"Ni nani aliyemtangulia Sheikh katika makatazo haya?"**

[1] Mfasiri: Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad
Tarehe 22 November, 2012 CE, Mukhtasari kutokamana na darsa ya Sheikh kwenye Masuali/Jawabu.
Darsa yenyewe inapatikana hapa:
http://mashhoor.net/
http://al-rahmah.net/misc/snips/

NI NANI ALIYEMTANGULIA IMÂM AL-ALBÂNI KUHUSU MAKATAZO YA KUFUNGA SIKU YA JUMAMOSI HATA KAMA LAU ITAANGUKIA KATIKA SIKU YA ĀSHÛRA AU SIKU YA 'ARAFAH?

Sisi tulikuwa tukishikilia kauli za ujumla zilizotajwa kwenye vitabu vya wanavyuoni. Kwahivyo kwa mfano, at-Twahawi alipokea kutoka kwa baadhi yao (wanavyuoni) kuhusu makatazo ya kufunga katika siku za Jumamosi. Ibn Rushd, tena kuorodhesha kwake kukawa ni kwa kina, amesema: **"Swaumu ziko katika sampuli mbili: harâm na wâjib na yaliyo harâm nayo yako katika sampuli mbili: yaliyoafikiwa na yaliyokhitilafianwa."** Kisha akataja kuhusu sampuli za swaum zilizokatazwa ambazo watu walizokhitilafiana kwazo na wala hakuyahusisha haya kwa yoyote. Sheikhul Islâm, katika "Iqtidhâ' Swirâtal Mustaqîm" alipokea kutoka kwa baadhi ya marafiki za Imâm Ahmad kuhusu kuchukia kufunga katika siku za Jumamosi. Mas'ala yakabaki katika njia hii ya ki-Ujumla. Baad ya kifo cha Sheikh [al-Albâni, *rahimahullâh*] katika mwaka wa 2008 CE/1429 AH, kwa mategemezi ya uhakika, Wizara ya Mali za Wakfu katika nchi ya Qatar, walichapisha kitabu chenye kusherehesha *"Sherh Ma'âni al-Athar"* [Imâm at-Twahâwi] cha al-'Ayni kiitwacho – *"Nukhab al-Afkâr fi tanqîh Mabânî il-Akhbâr fi Sharh Ma'âni il-Athar"*[2]. Katika mjalada wa Nane, ukurasa wa 433, aliposema Abu Ja'far at-Twahâwi: **"[kundi la] watu wamejiegemeza juu ya hadîth hii na wakachukia sana kufunga swaum za Sunnah katika siku za Jumamosi."** Ni watu gani hawa? Hakuna anayejua, si Sheikh wetu [Imâm al-Albâni, *rahimahullâh*] wala mtu yoyote kabla ya kuchapishwa na kutangazwa kitabu hiki. Akasema Imâm al-'Ayni, mtunzi wa kitabu *"Umdatul Qâri."*

"Alikusudia kwa neno "[kundi la] watu...": Mujâhid, miongoni mwa wanafunzi wa Ibn 'Abbâs, Twâwus Ibn Kaysan, Ibrâhim an-Nakha'i na Khâlid Ibn Ma'dân."[3]

Subhânallâh! Mujâhid alikuwa ni mtu wa Makkah, Twâwus Ibn Kaysan alikuwa ni mtu wa Yemen, Ibrâhim an-Nakha'i alikuwa ni mtu wa Kûfah na Khâlid Ibn Ma'dân alikuwa ni mtu wa Shâm. Maana yake ni kwamba: Kulikuwa na kundi la *Ma-Tâbi'in* waliotawanyika katika sehemu za Makkah, Kûfah, Yemen na Shâm katika zama za baada ya Maswahaba waliokuwa ni ma-Imâm wakubwa, ma-Imâm Wanne wakubwa wa Ma-Tâbi'in ambao waliochukia kufunga siku za Jumamosi iwapo inakuwa si swaum ya wâjib, na wametumia kama dalili hadîth iliyotangulia kutajwa hapo awali, na baadhi yao wameisimulia hadîth hiyo. At-Twahâwi ameipokea hadîth hiyo kwa njia ya Khâlid Ibn Ma'dân, kutoka kwa 'Abdillâh Ibn Busr, naye kutoka kwa Dadake as-Sam'â, aliyesema: *"Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliniambia: 'Usifunge siku za Jumamosi isipokuwa zile ambazo Allâh alizokufaradhishieni na lau mmoja wenu asipate chochote cha kula isipokuwa gamba la mti, basi na alitafune hilo.'"*. Hii ndiyo rai ya wale ambao waliokataza [kufunga katika siku za Jumamosi]. Na haya ndiyo maandiko yaliyopokewa, riwaya za wapokezi na riwaya za Ma-Salafi zinavyoashiriya, na ndiyo rai waliyokuwa nayo baadhi ya wanavyuoni.

Mimi nashangazwa na kundi la baadhi ya wasomi, na baadhi ya ma-Imâm wa Misikiti, ambao ilimu zao bado ni changa, wao hawana tahadhari na katika kila

[2] Imefanyiwa Tahqîq na Abu Tamîm Yâsir bin Ibrâhîm
[3] Rejea kwenye Chapa asili hapa:
http://www.qssea.net/Ebooks/Nukhabu.pdf

mas'ala ambayo ndani yake muna ikhtilafu basi wao hujiepusha nayo, lakini linapokuja suala la kufunga katika siku ya Jumamosi, utakuta wao tayari washawasimanga wenzao kuwa ni wazushi, wakiwashambulia wenzao kwa maneno makali na kuanza kushuku niya za watu. Sheikh wetu, [Imâm al-Albâni, *rahimahullâh*] alikuwa na msimamo wa misingi ya wanavyuoni, na dalili zake zilikuwa zimekita mizizi na ni nzito, na imekurubia kukosa mtu yoyote atakayekaa pamoja naye kwenye mkusanyiko wa halaiki ya watu isipokuwa utamkuta akisalimu amri kutokana na dalili zake.

Baadhi ya Mashekhe wa Madinah walinipasha habari yakwamba, Sheikh Swâleh, twamuomba Allâh Amuhifadhi na Amzidishie maisha, **"Alikuja Sheikh al-Albâni na hapo ndipo mara ya kwanza tuliposikiya kuhusu makatazo ya kufunga katika siku za Jumamosi. Walikaa naye Maskhekhe wa Madina. Watu wakaanza kunakishiana naye, mpaka baadhi yao wakaanza kupaaza sauti zao.[4] [Imâm al-Albâni] akajibu kwa kuwaambia, 'hebu tulieni, dalili na ushahidi...' kisha Sheikh akaanza kuwabainishia."** Alipoanza kuyafafanua mas'ala, Sheikh Swâleh akasema, jina lake jingine limenitoweka kwa sasa...

[Akatoa uzindushi mmojawapo]: "Sheikh Swâeh as-Suhaymi."

Sheikh Mash-hur: "Naam, Sheikh Swâeh as-Suhaymi, Allâh Akuhifadhi", ndugu Ya'qûb alikuwa akimsomea Sheikh katika Masjid an-Nabawi. Sheikh Swâeh as-Suhaymi (*hafidhahullâh*) akasema pindi alipokuwa amekaa na Sheikh [Imâm al-Albâni, *rahimahullâh*]: "Mimi nasema kama unayoyasema wewe, na itakuwaje nisiyaseme hayo?!" Kisha wa pili na mara wa Tatu naye, wote wakasema kauli kama hiyo. Kiyasi cha kwamba baadhi ya wanavyuoni wakasema, kumwambia Sheikh [Imâm al-Albâni, *rahimahullâh*]: **"Twamshukuru Allâh kwa kukufanya wewe kuwa ni Salafi na Hakukuwacha kuwa ni Hanafi!"** Kwahivyo yanayoweza kujitokeza hapa ni kwamba: Mbinu ambazo alizozitumia Sheikh kwa kuifikia rai ya makatazo ya kufunga swaum [isiyokuwa ya faradhi] ni mbinu maarufu iliyothubutu kimsingi na iliyopitiwa na *Ma-'Ulamâ'* kwenye mas'ala chungu nzaima.

Sheikh [Imâm al-Albâni, *rahimahullâh*] alizichukulia riwaya na umuhimu mkubwa sana pamoja na hadîth na alikuwa akisema: **"Mimi nashikamana na uswahihi wa hadîth"** na akatunga kitabu akakiita "*al-Hadîthu Hujjatun bi nafsihi*" [Hadîth ndiyo hoja yenyewe]. Alikuwa akiwapinga wale waliokuwa wakisema: **"Hadîth**

[4] Baadhi ya mijadala hii yanaweza kusikika katika vikao vilivyosajiliwa juu ya mas'ala ya makatazo kuhusu kufunga swaum za Sunnah katika siku za Jumamosi yaliyofanyika baina ya Imâm al-Albâni (*rahimahullâh*) na Muhaddith wa Madinah, al-'Allâmah 'AbdulMuhsin al-'Abbâd al-Badr (*hafidhahullâh*). Wakati Imâm al-Albâni na al-'Allâmah 'AbdulMuhsin al-'Abbâd al-Badr walipokuwa wakiendelea na mdahalo wao ulioegemezwa juu ya 'Ilmu, idadi ya watu waliokuwa wakishuhudia tukio hilo walianza kuingilia katika majadiliano hayo mara kwa mara ili wadhihirishe upinzani wao kwa Imâm al-Albâni (*rahimahullâh*).

Rejea katika usajili wa Youtube kuhusiana na Mdahalo wenyewe hapa:
https://www.youtube.com/watch?v=yyrxNFn2ilc

inakuwa ni hoja tu iwapo watu watatekeleza kulingana na mafunzo yake, lau watu watawacha kuitekeleza kulingana na mafunzo yake basi haitokuwa ni hoja." Haya ni matamshi ya upotofu, kwani maadamu hadîth ni swahih, basi hadîth hiyo inakuwa ndiyo hoja na dalili yenyewe. Tahadhari, alikuwa akipenda kusema Sheikh, **"Inalazimu kupatikane baadhi ya watu wenye 'Ilmu waliotekeleza kulingana na mafunzo yake."** Alikuwa akiongezea juu ya hayo, **"Endapo tuwe twaijua au tusiijue."** Yeye hakujua kuwahusu wale waliotekeleza kulingana na mafunzo yake [hadîth hiyo] ya kutofunga Swaum za Sunnah katika siku za Jumamosi[5] na pindi sisi tulipokuwa tukiulizwa: "hebu tutajieni watu waliokuwa wakikataza kufunga siku za Jumamosi", tulikuwa hatujui, na tulikuwa hatujui kuwataja wale waliokataza isipokuwa kwa kupitia kwenye kitabu hiki [*yaani; Nukhab al-Afkâr fi tanqîh Mabânî il-Akhbâr fi Sharh Ma'âni il-Athar*]. Lakini juu ya yote hayo, kabla ya kitabu hiki kuchapishwa, ambacho kilichochapishwa hivi karibuni, takriban miaka michache iliyopita, katika mwaka wa 2008, mimi najikomboa nafsi yangu na kukiri yakwamba sina kitabu hicho, na kama walivyo wengine tena walionizidi mimi ki-'ilmu, na walio katika daraja ya sawa na Masheikh zangu, na wao wanaruhusu kufungwa siku za Jumamosi. Lau kama utapambana na mtu unayenasibiana naye katika jamii yako, au mtu umpendaye, au jirani yako, usimkashifu kwa kukikosa [kitabu hicho], bali mkashifu mwenye kuyapinga makatazo ya kufunga katika siku za Jumamosi. Kwa sababu suala lime-egemezwa juu ya Usûl. Lakini hata hivyo, kulikomboa suala hilo kwa misingi na *istinbât* na *istidlâl* na watu wenye kukataza ni mas'ala mapana mno.

Natumai yakwamba mumeyahifadhi haya kutoka kwangu, na hapa namalizia darsa yangu kwa maneno haya: Hadîth ni hoja ya kujitosheleza yenyewe. Uswahih wa hadîth hautegemezwi juu ya watu katika kutekelezwa kwake, kwahivyo iwapo watu wataitekeleza [hadîth hiyo], basi hilo ni jambo linalofaa, na iwapo watu hawatoitekeleza [hadîth hiyo], itakuwa ni jambo la makosa. Vilevile hapana hadîth yoyote isipokuwa paliwahi kuwa na baadhi ya Ma'Ulamaa na watu wema waliowahi kuitekeleza. Lakini, juu ya yote hayo, ukosefu wa kuijua [hadîth hiyo] hakuwajibishi kukosa kuitekeleza [kulingana na hadîth yenyewe]. Ikiwa sisi hatuijui hadîth yenyewe, hili haliwajibishi yakwamba hakuna aliyewahi kutekeleza kulingana na hadîth yenyewe. Kwahiyo, Imâm at-Tirmidhi katika mwanzoni mwa kitabu chake, *al-'Ilal as-Swaghîr* na mwishoni mwa ukusanyaji wake, kilicho maarufu kwa jina la *as-Sunan*, amesema:

"... yote yaliyomo ndani ya kitabu as-Swahih yameshatekelezwa na wanavyuoni isipokuwa kwa hadîth mbili: kuunganisha baina ya swala mbili; na ya pili ni hadîth ya mtu mwenye kunywa mvinyo [tembo]. Iwapo atakunywa kwa mara ya pili au ya tatu, basi muuweni."

[5] Lakini hata hivyo, Imâm al-Albâni (*rahimahullâh*) alimwambia Muhaddith wa Madinah, al-'Allâmah 'AbdulMuhsin al-'Abbâd al-Badr (*hafidhahullâh*) wakati walipofanya mdahalo wao, yakwamba aliyemtangulia yeye katika rai ni Swahaba aliyeipokea Hadîth yenyewe! Na kwamba iwapo atakubalika yeye yakwamba alikuwa ni Mwanachuoni, kwahivyo yeye ndiye aliyemtangulia Imâm al-Albâni (*rahimahullâh*) katika rai hiyo.

NI NANI ALIYEMTANGULIA IMÂM AL-ALBÂNI KUHUSU MAKATAZO YA KUFUNGA SIKU YA JUMAMOSI HATA KAMA LAU ITAANGUKIA KATIKA SIKU YA ĀSHÛRA AU SIKU YA 'ARAFAH?

Imâm at-Tirmidhi akasema yakwamba ahâdîth hizi mbili ndizo ambazo hazijawahi kutekelezwa. Hali sio kama hivyo alivyosema kwani mimi nimeyajadili kwa urefu katika kitabu changu *al-Jam' Bayna as-Swalatayn* [kujumuisha baina ya Swala mbili] kuwahusu wale waliowahi kutekeleza kulingana na hadîth ya kujumuisha baina ya swala mbili [haliyakuwa ni wasafiri au wakaazi wa mji, na pindi inaponyesha mvua] kabla ya at-Tirmidhi. Vilevile al-'Allâmah Ahmad Shâkir, katika Musnad ya Imâm Ahmad, aliichambua hadîth kuhusu kumuuwa mtu mwenye kuendelea kurudia unywaji wa *khamr* kwa mara ya Tatu au ya Nne, na akalibainisha suala hilo kwa urefu, mpaka akaandika Makumi ya Kurasa yaliyofikia takriban kurasa Sabiini akithibitisha yakwamba kundi na *Ma-Tâbi'în*, na wale waliokuja baada yao, walitekeleza kulingana na hadîth ya kumuuwa mwenye kushikilia kuendelea kunywa *khamr* baada ya kukemewa mara ya Tatu na Nne. Kisha Allâh akamrahisishia kukichapisha kando aliyoyanukuu kutoka katika Musnad ya Imâm Ahmad katika kijitabu kidogo kwa jina la *Kalimat ul-Fasli fi Qatl Mudmin il-Khamr* [Neno lililo sheheni linalohusiana na Kuuwawa kwa Mlevi]. Sisi hatujui hata hadîth moja ya Mtume (*Swallallâhu 'alayhi wasallam*) ambayo haikuwahi kupata kutekelezwa, lakini wakati mwengine huwenda tusiwajue watu waliowahi kutekeleza kulingana na hadith. Kwahivyo, hifadhini kutoka kwangu: **'Hadîth ni hoja ya kujitosheleza yenyewe. Na utekelezaji kulingana na hadîth umethubutu hata kama sisi hatujui kuhusiana nayo [hiyo hadîth].'** Allâh yanamuelea Zaidi."

Swala na Salamu Zimshukie Mtume wetu Muhammad, Aali zake na Maswahaba zake wote.